



Jina langu ni Ndalo.



Mimi hupenda  
kusoma hadithi.




Baba yangu  
anamfuga  
ng'ombe.

Anaitwa Pendo.



Mimi ninampenda  
Pendo.




Pendo hupenda  
kula nyasi siku  
nzima.



Pendo pia hunywa  
maji mengi.



Wakati mwingine  
baba humpa  
Pendo nafaka.



Baba humkama  
Pendo.

Sisi humtunza  
Pendo naye  
hutusaidia.





Pendo hutupa  
maziwa mengi.



Baba huuza  
maziwa.

Hutumia pesa hizo  
kuninunulia vitabu  
vya hadithi.



Mimi hunywa  
maziwa mengi.



Umefahamu kwa  
nini ninampenda  
ng'ombe wetu  
Pendo?